



CHUO CHA UALIMU KING'ORI

CHUO KIPO: PHILIPS-Banana/SEKEI,

Barabara ya Moshi –Arusha. UMBALI: Mita mia moja (m 100) kutoka barabara kuu.

+255754255888 ✉ S.L.P. 708, Arusha, TZ. ✉ kingoriteachers@yahoo.com, 🌐 www.kingoriteachers.com

MAELEKEZO, MAAGIZO NA MASHARTI YA KUJIUNGA NA CHUO CHA UALIMU KING'ORI

Maelekezo:

Chuo cha Ualimu King'ori ni chuo cha kutwa na Bweni. Chuo kinatoa mafunzo ya Ualimu ngazi ya Diploma. Tunafuata Mitaala na Mihutasari iliyokubaliwa na Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia. Chuo kimesajiliwa na NACTVET kwa usajili REG/TLF/099 na Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia kwa usajili wa CU118. Vilevile, tumesajiliwa kwa usajili wa Baraza la Mitihani Tanzania E0623. Chuo kinawaandaa wanachuo ili wawe walimu bora katika Shule za Msingi na katika jamii kwa ujumla.

Mahali Chuo Kilipo

Chuo cha Ualimu King'ori kipo katika mtaa wa **Banana** (Sekei), maeneo ya **Phillips**, mkoani **Arusha**. Kipo mita 100 kutoka barabara ya Arusha-Moshi kando ya barabara iendayo Mahakama ya Wilaya ya Sekei.

Maelekezo Afya

- a) Ili ukubaliwe kusomea Ualimu utahitajika kupimwa Afya yako na kuthibitishwa na daktari wa Serikali kwa kujaza fomu (Request for Medical Examination) iliyoambatanishwa kwenye fomu hii. Itakupasa uje na fomu hii ujapo chuoni. Hakikisha kuwa fomu hiyo imegongwa muhuri wa Ofisi na Daktari husika.
- b) Pia chuo kinasisitiza kuwa wanachuo walio na bima za afya ni muhimu waje na kadi zao za bima kwani zitakuwa msaada kwao pindi watakapougua wakiwa chuoni.

- Kwa wale wasiokuwa na bima ya afya, chuo kinawashauri kukata bima ya muda (Mwaka mmoja) ili iwasadie pindi wanapohitaji matibabu. Bima hii mwanachuo anaweza kukata katika mifuko ya bima ya afya katika mkoa anaotoka kwa gharama ya 50,400 Tsh.

Kufungua Chuo

- (a) Chuo kitafunguliwa tarehe **01/07/2026** kwa ajili ya wiki ya maelekezo (Orientation week) pamoja na kukamilisha Usajili kwa wale ambao watakuwa bado hawajakamilisha. Mafunzo ya Ualimu yataanza rasmi tarehe **06/07/2026** baada ya wiki hiyo ya maelezo na kukamilisha usajili. Unatakiwa uwe umekamilisha usajili wako kabla ya tarehe **06/07/2026**
- (b) Elewa kuwa nafasi za kusomea Ualimu ni chache na zinatafutwa na Watanzania wengi, hivyo, UKISHINDWA KUWASILI CHUONI WIKI MOJA BAADA YA TAREHE YA KUFUNGUA CHUO, HUTAPOKELEWA.

TANBIHI: Kama kutakuwa na mabadiliko ya tarehe ya kufungua chuo, utajulishwa kwa njia ya simu au Kupitia tovuti ya chuo.

Utambulisho:

Ili kuthibitisha kuwa wewe ndiye HALISI ambaye unajiunga na mafunzo ya Ualimu katika chuo hiki, itakubidi uje na viambatanisho vifuatavyo;

- a) Cheti halisi cha kumaliza mafunzo/elimu ya kidato cha IV , VI (Original School Leaving Certificate) kikionyesha shule uliyosoma na cheti halisi cha matokeo ya mitihani ya kidato cha IV VI cha Baraza la Mitihani la Taifa (BMT) au "Original Result slip" na vivuli vyake (photocopy) ambavyo vitabaki kwenye faili lako.
- b) Nakala **mbili** (2) za picha yako ndogo (passport size) za rangi, ulizopiga hivi karibuni.

Kusajiliwa

Ili usajiliwe ni lazima uje na mahitaji yafuatayo;-

- a) Barua ya kuitwa kujiunga na chuo tuliyokutumia (Joining Instructions).
- b) Spring file moja kwa ajili ya kuweka nakala ya vivuli vya vyeti vyako.
- c) Fomu ya kupimwa na kuthibitisha afya yako ikiwa imejazwa na kutiwa sahihi na muhuri wa daktari aliyekupima.
- d) Fomu ya kujiunga na chuo ikiwa imejazwa kikamilifu na wewe mwenyewe na mzazi/mlezi, mwajiri/mfadhili wako.(MKATABA BAINA YA MWANACHUO NA CHUO).
- e) Mahitaji binafsi yafuatayo :

✓ Viatu vyeusi vya shule.
✓ Ream mbili (2) za A4 moja kila mwaka.
✓ Daftari 12 kwa ajili ya masomo mbalimbali.
✓ Jezi ya rangi ya bluu bahari (Bukta na tisheti) kwa ajili ya mazoezi.
✓ Viatu (raba) vya kufanyia mazoezi.
✓ Godoro (School size). (<i>Kwa wanachuo wa hostel</i>)
✓ Shuka mbili (rangi ya bluu), mto, foronya na blanketi. (<i>Kwa wanachuo wa hostel</i>)
✓ Taulo, chandarua na ndoo ya maji (<i>Kwa wanachuo wa hostel</i>).
✓ Kijiko, kikombe na sahani kwa ajili ya chakula.

Mawasiliano

Taarifa zote muhimu kwa mfano: maafa, msiba, ugonjwa n.k toka nyumbani lazima zipitie kwa Mkuu wa Chuo na siyo kwa mwanachuo moja kwa moja. Wazazi/ walezi / waume / wake / ndugu, wote wanapaswa kuzingatia utaratibu huu wa mawasiliano.

Masharti Mengine Muhimu

A. Taaluma

Chuo kinaweka msisitizo wa kipekee katika maendeleo ya wanachuo wake kitaaluma. Kiwango cha kufaulu kwa wanachuo katika kila somo ni alama 50. Kwa wanachuo wa michepuo yote, endapo utashindwa kufikia kiwango hicho mwishoni mwa muhula wako wa kwanza utalazimika kufanya mtihani wa marudio (Suplimentary Examination). Ukishindwa tena mtihani huo, utashauriwa utafute kozi nyingine tofauti na Ualimu.

Vilevile tunao walimu wakutosha na mahiri katika ufundishaji. Mitihani hii ni njia mojawapo ya kuinua UBORA NA HADHI YA UALIMU NCHINI. Hivyo mwanachuo anashauriwa aje chuoni akiwa anajielewa fika kuhusu uwezo wake wa kumudu masomo atakayo chukua. Atatakiwa aweke mkazo kwenye masomo tangu siku anapoingia chuoni.

Pia, wanachuo watapewa utaratibu na mwongozo wa kufanya mazoezi ya kufundisha (BTP) wanapokuwa chuoni.

B. Kanuni za Chuo

Pamoja na masharti haya na maagizo ya kujiunga na chuo utapewa kanuni za kukusaidia kuishi vizuri hapa chuoni. Hakikisha umezisoma, umezielewa, na unakubaliana nazo kabla ya kusajiliwa.

C. Ada

Ulipaji wa Ada ya Chuo umegawanywa kama inavyoonekana kwenye jedwali hapo chini, kumrahisishia Mwanachuo / Mzazi / Mlezi ulipaji. Mwanachuo / Mzazi / Mlezi anaweza kulipa Ada yote ya mwaka mzima bila kujali mgawanyo huu.



CHUO CHA UALIMU KING'ORI

CHUO KIPO: PHILIPS-Banana/SEKEI,

Barabara ya Moshi –Arusha. UMBALI: Mita mia moja (m 100) kutoka barabara kuu.

+255754255888/ +255786263831, S.L.P. 708, Arusha, TZ. kingoriteachers@yahoo.com, www.kingoriteachers.com

FOMU YA KUJIUNGA NA CHUO CHA UALIMU KING'ORI

A. TAARIFA BINAFSI.

- i. Jina kamili:
 ii. Anuani
 iv. Mkoa
 vi. Jina la Mzazi/Mlezi:
 (iii) Simu:
 (v) Wilaya:
 (vii) Simu :

B. KIWANGO CHA ELIMU

- (i) Shule ya Msingi Mwaka: Mpaka:
 (ii) Shule ya Sekondari Mwaka: Mpaka:
 (iii) Elimu ya Chuo (Kwa waliosoma tu):

C. UTHIBITISHO

Mimi nathibitisha kuwa taarifa nilizojaza hapo juu ni sahihi.
 Jina Sahihi Tarehe

Maelekezo Muhimu: Utakaporudisha fomu hii tafadhali wasilisha vivuli vya vyeti vyako vinavyoonesha matokeo kama ulivyojaza awali. Taarifa hizi zitabaki katika faili lako. Wakati wakuripoti chuoni utalazimika kuonyesha cheti halisi kwa uhakiki.

Kwa Matumizi ya Ofisi tu

Maoni ya Mkuu wa Chuo :

Sahihi : Tarehe : Muhuri :

GOVERNMENT OF TANZANIA

REQUEST FOR MEDICAL EXAMINATION



CHUO CHA UALIMU KING'ORI

CHUO KIPO: PHILIPS-Banana/SEKEI,

Barabara ya Moshi –Arusha. UMBALI: Mita mia moja (m 100) kutoka barabara kuu.

+255754255888/ +255786263831, S.L.P. 708, Arusha, TZ. kingoriteachers@yahoo.com, www.kingoriteachers.com

Date /.../2026

The Medical Officer

.....

RE: MR/MRS/MISS: (Full name)

Please examine the above named as to his/her physical and mental fitness for a full time teacher training course

The examination should include the following category or sub-category of which will render the applicant ineligible in case of defect.

Pregnancy (category IV) will also render a girl candidate ineligible for the course.

- a) Eye sight:
- b) Hearing:
- c) Speech:
- d) Limbs:
- e) Venereal diseases:
- f) Leprosy:
- g) Peptic ulcers:
- h) Epilepsy:
- i) Tuberculosis:
- j) Other serious diseases:
- k) Pregnancy:

Signature:

Date:

Official stamp: